

# العقيدة الصحيحة

## ( باللغة السواحلية )

تأليف  
الشيخ / عبد العزيز بن عبد الله

ترجمة  
أميوناً أحمد أوراري



Conveying Islamic Message Society  
P.O. Box 834 - Alex - Egypt  
E-Mail: info\_en@islamic-message.net  
E-Mail: cims\_eg@yahoo.com  
Site: www.islamic-message.net  
Not for sale نهري وللربيع

*ITIKADI SAHIHI*

*Mtungaji*  
*Sheikh Abdulaziz Abdallah Ibn-Baaz*

*Mfasiri*  
*Mbwana Ahmad Urari*

العقيدة الصحيحة

(باللغة السواحلية)

تأليف

الشيخ / عبد العزيز بن عبدالله بن باز رحمه الله

ترجمة

ابوانا أحمد اوراري



Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu pekee, na rehema na amani zimfikie Mtume ambaye hakuna Mtume mwengine baada yake. Pia rehema na amani ziwafikie Jamaa na Swahaba wake.

Kwa kuwa itikadi sahihi ndio msingi wa dini ya Kiislamu, nimeonelea iwe ndio maudhui ya mhadhara huu.

Ni jambo lenye kujulikana kwa hoja za kisheria katika Qur'ani na Sunna<sup>i</sup> kwamba, matendo na maneno yanakubaliwa pale tu yanapotokana na itikadi sahihi. Iwapo itikadi sio sahihi, basi matendo na maneno yanayotokana na itikadi hiyo ni batili, kama Mwenyezi Mungu alivyosema kuwa: "*Na ye yote anayeikufuru (anayeikataa) imani, basi yameporomoka (yamepotea bure) matendo yake (ya kheri) na ye yeye huko akhera (atakuwa) ni mi ongoni mwa wenyе hasara*".<sup>ii</sup>

Pia amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Na hakika, umeshushiwa wahyi (ufunuo) wewe (Mtume Muhammad) na (Mitume wengine) waliokuwepo kabla yako kwamba, ukishirikisha (ukifanya shirki) basi yataporomoka (yatapotea bure) matendo yako (japo ni mema) na kwa yakini utakuwa mi ongoni mwa wenyе hasara*".<sup>iii</sup> Aya za Qurani katika kuelezea maana hii ni nyingi.

Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume wake Muaminifu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, zinafahamisha kwamba, itikadi sahihi, kwa ufupi,



inapatikana katika kumwamini :1) Mwenyezi Mungu 2) Malaika wake 3) Vitabu vyake 4) Mitume wake 5) Siku ya Mwisho na 6) Qadari; kheri na shari yake. Mambo haya sita ndio misingi ya Itikadi sahihi ambayo kimeshuka nayo kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa Itikadi hiyo, Mwenyezi Mungu amemtuma Mtume wake Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Yanachipuka kutokana na misingi hii mambo yote ya Ghaibu <sup>iv</sup> yanayopasa kuaminiwa na mambo yote aliyyatolea habari Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Hoja za misingi hii sita ni nyingi sana. Mionganoni mwa hoja hizo ni neno la Mwenyezi Mungu aliyetakasika lisemalo kuwa: "*Sio wema kuzielekeza nyuso zenu tu upande wa mashariki na magharibi (katika sala) lakini (wema) ni (wa) ambaye amemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Vitabu na Mitume*".<sup>v</sup>

Na kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika inayosema kwamba: "*Mtume ameyaamini yaliyoteremshwa kutoka kwa Mola wake na waumini (pia wameyaamini). Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi kati ya yeyote katika Mitume wake*".<sup>vi</sup>

Na kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika isemayo kuwa: "*Enyi ambao mmeamini, muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kitabu ambacho amekiteremsha kwa Mtume wake na vitabu ambavyo ameviteremsha huko nyuma. Na yeyote anayemkufuru (anayemkana) Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu*

شبكة الألوكة - قسم الكتب

*vyake na Mitume wake na Siku ya Mwisho, basi amepotea upotevu ulio mbali".<sup>vii</sup>*

Na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "Hivi hujui kuwa Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo katika mbingu na ardhi? Bila shaka hayo yapo katika kitabu. Bila shaka hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi".<sup>viii</sup>



Ama Hadithi sahihi (za Mtume) juu ya misingi hii ni nyingi sana. Miongoni mwa Hadithi hizo ni Hadithi mashuhuri aliyopokea Imam Muslim katika kitabu chake 'Sahih Muslim' katika Hadithi ya kiongozi wa waumini Omar bin Al-Khattaab, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba Jibrili alimuuliza Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuhusu imani na Mtume akamjibu kwa kusema kuwa: " (Imani) Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya Mwisho na kuiamini Qadari; kheri yake na shari yake".<sup>ix</sup>

Kutokana na misingi hii sita yanachipuka mambo yote yanayompasa Muislamu kuyaitakidi katika haki ya Mwenyezi Mungu na katika mambo ya Akhera na yasiyokuwa hayo mionganoni mwa mambo ya Ghaibu.

## 1. KUMUAMINI MWENYEZI MUNGU

Ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu kuamini kuwa yeye ndiye Mungu wa kweli, anayestahiki kuabudiwa badala ya kila kisichokuwa yeye, kwa sababu yeye ndiye Muumba wa waja, Mfadhili wao, Mwenye kuzisimamia riziki zao, Mwenye kuzijua siri na dhahiri zao, Mwenye uwezo wa kumpa thawabu mwenye utiifu na kumuadhibu mwenye kufanya uasi. Kwa ajili ya kuabudu huku, ndio



Mwenyezi Mungu ameumba watu na majini na kuwaamuru hivyo, kama Mwenyezi Mungu aliyetukuka alivyosema kuwa: "Na sikuumba majini na watu isipokuwa tu kwa kutaka (wawe) wananiabudu. Sitaki kutoka kwao riziki yoyote na wala sitaki wanilishe. Bila shaka, Mwenyezi Mungu ndiye tu Mtoaji riziki, Mwenye nguvu, Mwenye nguvu kubwa".<sup>x</sup>

Na amesema Mwenyezi Mungu aliyetakasika kuwa: "Enyi watu, muabuduni Mola wenu ambaye amekuumbeni nyinyi na (amewaumba) waliokuwepo kabla yenu ili mpate kuokoka. (Mwenyezi Mungu) Ambaye amewafanyieni ardhi kuwa ni busati na mbingu kuwa ni paa na akateremsha kutoka mawinguni maji (mvua) ambayo akatoa (akaotesha) kwa maji hayo riziki zenu katika matunda. Hivyo basi msimfanyie Mwenyezi Mungu washirika na ilhali nyinyi mnajua (kuwa Mwenyezi Mungu hana mshirika)".<sup>xi</sup>

Mwenyezi Mungu amewatumua Mitume na ameteremsha vitabu ili kuiweka wazi haki hii, kuilingania (kuihubiri) na kuyatahadharisha yale yanayopingana na haki hii, kama Mwenyezi Mungu aliyetakasika alivyosema kuwa: "Na hakika, tulipeleka katika kila umma (taifa) Mtume (ili awafundishe watu) kwamba muabuduni Mwenyezi Mungu na jiepusheni na Taghuti".<sup>xiii</sup>

Na amesema Menyezi Mungu kuwa: "Na hatukupeleka kabla yako Mtume yeyote ila (tulikuwa) tunampa wahyi (ufunuo) kwamba hakuna

*mwenye haki ya kuabudiwa ila mimi (Mwenyezi Mungu) tu, hivyo niabuduni".<sup>xiv</sup>*

Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "[Hiki] Ni kitabu [ambacho] zimetengenezwa vizuri aya zake kisha zimefanuliwa vyema kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwenye hekima, Mwenye ujuzi (wa kila jambo ili) kwamba msimuabudu (yeyote) isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Hakika, mimi kwenu ni muonyaji, mtoaji habari njema kutoka kwake".<sup>xv</sup>

Uhakika wa kuabudu ni kumkusudia Mwenyezi Mungu pekee kwa yote ambayo amewataka waja wamuabudu kwayo, ikiwa ni pamoja na kuomba, kuogopa, kutaraji, kusali, kufunga, kuchinja, kuweka nadhiri na aina nyingine za Ibada zisizokuwa hizo. Inatakiwa kumfanyia Mwenyezi Mungu tu Ibada hizo kwa njia ya kumnyenyeka, kutaraji rehema zake, kuogopa adhabu yake pamoja na kumpenda yeye Mwenyezi Mungu kikamilifu na kuunyenyekea utukufu wake.

Sehemu kubwa ya Qurani Tukufu imeshuka ili kuufafanua msingi huu mkubwa, kama kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika isemayo kwamba: "*Basi muabudu Mwenyezi Mungu ukimtakasia yeye tu dini. Ee, ni ya Mwenyezi Mungu tu dini iliyo takasika*".<sup>xvi</sup> Na kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: "*Na amehukumu Mola wako kwamba msiabudu (chochote) ila yeye tu*".<sup>xvii</sup>

Na kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: "*Basi muombeni (muabuduni) Mwenyezi Mungu mkimtakasia yeye tu dini, wajapochukia makafiri*".<sup>xviii</sup>

Katika 'Sahiih Bukhaariy' na 'Sahiih Muslim' imepokewa kwa Muaadh bin Jabal, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, akisema kwamba Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Haki ya Mwenyezi Mungu iliyopo kwa waja ni kwamba (wanatakiwa) wamuabudu yeye na wasikishirikishe naye kitu chochote*".<sup>xix</sup>

Ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu kuyaamini yale yote aliyoyafaradhisha kwa waja wake, ikiwa ni pamoja na nguzo tano za Uislamu ambazo ni:

- 1) Kukiri moyoni na kutamka kinywani kwamba, hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu na kwamba, Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.
- 2) Kusimamisha Sala.
- 3) Kutoa Zaka.
- 4) Kufunga Ramadhan.
- 5) Kuhiji Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu kwa mwenye uwezo wa kuiendea.

Pia ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu kuziamini faradhi nyingine zisizokuwa hizo na ambazo zimeletwa na sheria tukufu ya Kiislamu.

Muhimu na kubwa zaidi katika nguzo hizi tano ni ile ya *kukiri kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu tu na kwamba Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni Mtume wa Mwenyezi Mungu*. Kukiri huku kunataka ibada ifanywe kwa nia safi ya kumkusudia Mwenyezi Mungu pekee na kutomfanyia mwengine asiyekuwa yeye. Hii ndio maana ya 'Laa ilaaha il-



Lallaah', kwani maana yake ni: 'Hakuna muabudiwa wa haki ilia Mwenyezi Mungu tu'. Vyote vinavyoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu, iwe ni mwanadamu au malaika au jini au kingine kisichokuwa hivyo, basi hivyo vinaabudiwa kwa batili. Muabudiwa wa haki ni Mwenyezi Mungu pekee, kama Mwenyezi Mungu alivyosema kuwa: "*Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye tu (Mungu wa) haki na vile (vitu ambavyo watu) wanaviomba (wanaviabudu) badala yake (Mwenyezi Mungu) ndio tu batili*".<sup>xx</sup>

Umeshapita ufanuzi wa kwamba Mwenyezi Mungu aliyetakasika amewaumba wanadamu na majini kwa ajili ya msingi huu wa kumuabudu yeye tu, amewaamuru kuutekeleza, amewatuma Mitume wake kwa msingi huo na kuviteremsha vitabu vyake kwa msingi huo. Lizingatie hilo vizuri na kulitafakari ili ukudhihirikie ujinga mkubwa wa kutoujua msingi huu; ujinga ambao wametumbukia katika ujinga huo Waislamu wengi mpaka wakaviabudu vitu vingine pamoja na Mwenyezi Mungu na kuielekeza haki yake safi kwa asiyekuwa yeye. Mwenyezi Mungu ndiye wa kuombwa msaada!

Ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu aliyetakasika kuamini kuwa yeye ndiye Muumba wa ulimwengu, Mtengenezaji wa mambo ya walimwengu kwa ujuzi na uwezo wake kama anavyotaka, Mmilikaji wa dunia na akhera, Mola wa walimwengu wote. Hakuna Muumba wala Mola mwengine asiyekuwa yeye. Amewatuma Mitume na kuteremsha vitabu ili kuwafanya waja wawe wema na kuwalingania yale yenye uwokovu na wema kwao hapa duniani na akhera. Yeye Mwenyezi Mungu katika yote hayo hana mshirika, kama alivyosema kuwa: "*Mwenyezi*



*Mungu ndiye Muumba wa kila kitu na yeye juu ya kila jambo ni mtegemewa".<sup>xxi</sup>*

Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "Hakika, Mola wenu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana sawa juu ya Arshi. Anaufinika usiku kwa mchana huku ukiufuatia haraka haraka (na anaufinika mchana kwa usiku huku ukiufuatia haraka haraka) na (ameumba) jua na mwezi na nyota (vyote) vikiwa vimefanywa kuwa vitiifu kwa amri yake. Ee, ni kwake yeye tu kuumba na ni zake yeye tu amri. Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu (wote)".<sup>xxii</sup>

Ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu pia kuyaamini majina yake mazuri na sifa zake tukufu zilizopo katika kitabu chake kitukufu na zilizothibiti kunukuliwa kwa Mtume wake Muaminifu. Inapasa kuamini majina na sifa hizo bila ya kubadilisha maana (tahriif) au kukanusha maana (taatiil) au kuainisha namna (takyiif) au kufananisha (tamthiil). Bali inapasa majina na sifa hizo zithibitishwe kama zilivyokuja bila ya kufafanua umbile, pamoja na kuamini maana zake tukufu zinazofahamisha na ambazo ndio sifa za Mwenyezi Mungu aliyetukuka. Inapasa kumsifu Mwenyezi Mungu kwa sifa hizo katika njia inayofaa kwake bila ya kumfananisha na viumbe vyake katika sifa yoyote kati ya sifa zake, kama alivyosema kuwa: "*Hakuna chochote kama mfano wake na yeye ni mwenye kusikia, mwenye kuona*".<sup>xxiii</sup>

Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Basi msimpigie Mwenyezi Mungu a mifano. Hakika, Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui*".<sup>xxiv</sup>

Hii ndio itikadi ya Watu wa Sunna na Jamaa [Ahlus-Sunna Wal-jamaa = Suni] wakiwemo Swahaba wa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na waliowafuatia wao kwa wema. Hiyo pia ndio itikadi aliyoinukuu Imam Abul-Hassan Al-Ash'ary, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, katika kitabu chake 'Al-Maqalaat An-as-habil-hadiith Wa-ahlis-sunna' na pia wameinukuu wanazuoni wengine wenye elimu na imani.

Amesema Imam Al-Auzaaiy, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba aliulizwa Imam Az-Zuhriy na Mak'huul kuhusu aya za Qur'an zinazozungumzia sifa za Mwenyezi Mungu wakasema kuwa: "*Zipitisheni (zithibitisheni) kama zilivyokuja*".

Naye Waliid bin Muslim, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kwamba aliulizwa Imam Malik, Auzaaiy, Laith bin Saad na Sufian Ath-Thauriy kuhusu Hadithi za Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, zinazozungumzia sifa za Mwenyezi Mungu na wote, Mwenyezi Mungu awarehemu, walisema kuwa: "*Zipitisheni kama zilivyokuja, bila ya kuainisha namna*". Na Imam Auzaaiy, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: "*Tulikuwa tukisema, na ilhali Taabiina wapo, kwamba Mwenyezi Mungu aliyetakasika yuko juu ya Arshi yake na tunaziamini sifa za Mwenyezi Mungu zilizokuja katika Sunna za Mtume*".



Wakati alipoulizwa Rabia bin Abi-Abdulrahman Shekhe wa Imam Malik kuhusu kulingana sawa [kulikotajwa katika sura Al-Aaraaf (7) aya 54] alisema kwamba: "*Kulingana sawa kunajulikana na namna (aina) yake haijulikani na ujumbe unatoka kwa Mwenyezi Mungu na ni juu ya Mtume kuufikisha na ni juu yetu kuuamini*". Na Imam Malik, Mwenyezi Mungu amrehemu, alipoulizwa juu ya suala hilo la Mwenyezi Mungu kulingana sawa juu ya Arshi yake alisema kwamba: "*Kulingana sawa kunajulikana na namna yake haijulikani na kuamini ni wajibu na kuulizia ni uzushi (Bid'a)*". Halafu alimwambia yule mtu aliyemuuliza kwamba: "*Mimi sioni isipokuwa kwamba wewe ni mtu muovu tu*". Na aliamuru yule mtu atolewe nje.

Maana ya matamshi kama haya imepokewa pia kwa Mama wa waumini Ummu-Salamah [mke wa Mtume], Mwenyezi Mungu amuwiye radhi. Na Imam Abu-Abdulrahman Abdallah bin Al-Mubaarak amesema kuwa: "*Tunajua kuwa Mola wetu aliyetakasika yuko juu ya mbingu zake, juu ya Arshi yake, baidi (akiwa mbali) na viumbe vyake*".

Maneno ya Maimamu katika suala hili ni mengi mno. Haiwezekani kuyanuku yote katika mnasaba huu wa haraka. Yeyote anayetaka kufahamu zaidi katika suala hilo ayarejee yale waliyoyaandika wanachuoni wa Sun-nah, mfano:

- a) Kitabu 'As-sunnah' cha Abdallah bin Al-imam Ahmad.
- b) Kitabu 'At-Tawhid' cha Imam mkubwa Muhammad bin Khuzaimah.



- c) Kitabu 'As-Sunnah' cha Abul-Qaasim Alla'alikaaliy At-Tabariy.
- d) Kitabu 'As-Sunnah' cha Abu-Bakar bin Abi-Aasim.
- e) Jawabu la Sheikhul-Islaam Ibni-Taymiyah kwa watu wa Humaat.<sup>xxv</sup> Jawabu hilo ni adhimu na lenye faida sana. Katika jawabu hilo Sheikh, Mwenyezi Mungu amrehemu, ameweka wazi itikadi ya Watu wa Sunna na Jamaa. Amenkuu maneno yao mengi pia amenukuu hoja za kisheria na za kiakili juu ya usahihi wa waliyoyasema watu wa Sunnah na ubatili wa waliyoyasema wapinzani wao.

Vile vile kitabu cha Sheikh kiitwacho 'At-Tadmur-iyyah' ni adhimu pia, kwani amelieleza kwa urefu suala hili na kuifafanua itikadi ya Watu wa Sunna kwa hoja zake za kisheria na za kiakili. Pia amewajibu wapinzani kwa hoja zinazodhahirisha haki na kuivunja batili kwa mtu mwenye elimu, anayetafakari hayo kwa lengo jema na nia ya kutaka kujua haki.

Kila anayewapinga Watu wa Sunna (Suni) katika yale wanayoyaitakidi kuhusu majina na sifa za Mwenyezi Mungu, basi hapana budi atatumrukia katika kuzipinga hoja za kisheria na za kiakili pamoja na kutumbukia katika utata wa wazi katika anayoyathibitisha na kuyakanusha.

Ama Watu wa Sunna wao wamemthibitishia Mwenyezi Mungu yale ambayo Mwenyezi Mungu amejithibitishia katika Qur'an Tukufu au yale ambayo Mtume wake Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amemthibitishia Mwenyezi Mungu katika Sunna zake sahihi. Wamethibitisha uthibitisho usiokuwa na ufananisho na wamemuepusha Mwenyezi Mungu na kufanana na viumbe, muepusho usiokuwa na kukanusha

maana. Kwa kufanya hivyo, Watu wa Sunna wamesalimika na utata na wamezitekeleza hoja zote. Hii ndio kanuni ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika kwa mtu ambaye ameshikamana na haki ambayo kwayo Mwenyezi Mungu amemtuma Mtume wake, akatoa juhudini zake katika hilo na akamtakasia Mwenyezi Mungu nia yake katika kuitafuta haki hiyo ili Mwenyezi Mungu amuwezeshe kuifuata haki na kumdhahirishia hoja zake kama Mwenyezi Mungu alivyosema kuwa: "*Bali tunaitupa haki juu ya batili na hivyo (haki) inaivunja batili na mara batili hutoweka*".<sup>xxvi</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Na hawatakuletea mfano (wowote) isipokuwa tu tunakuletea haki na tafsiri nzuri zaidi*".<sup>xxvii</sup>

Na Imam Al-Hafidh Ibn-Kathiir katika tafsiri yake mashuhuri amesema maneno mazuri katika suala hili wakati akiifasiri kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika isemayo kuwa: "*Hakika, Mola wenu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana sawa juu ya Arshi*".<sup>xxviii</sup>

Ni vizuri hapa kuyanukuu maneno hayo kwa sababu ya faida yake kubwa. Amesema Al-Hafidh Ibni-Kathiir, Mwenyezi Mungu amrehemu, kwamba: "*Watu katika suala hili wana kauli nyangi sana. Hapa sio mahali pa kuzichambua isipokuwa tu sisi katika suala hili tunafuata madhehebu ya As-Salaf As-Saalih [Wema Waliotangulia]: Malik, Auzaaiy, Ath-thauriy, Al-laith bin Saad, Ash-shaafiy, Ahmad, Is-haaq bin Raahawieh na maimamu wengine wa Kiislamu wasiokuwa hao; wa zamani na wa sasa. Madhehebu hayo ni kuthibitisha majina na sifa za Mwenyezi*

*Mungu kama zilivyokuja bila ya kuainisha namna wala kufananisha wala kukanusha maana. Bali ilivyo ni kama walivyosema Maimamu, akiwemo Nuaim bin Hammaad Al-Khuzaaiy Sheikh wa Imam Bukhariy kwamba: Yeyote anayemfananisha Mwenyezi Mungu na viumbe vyake basi amekufuru na yeyote anayekanusha sifa alizojisifia Mwenyezi Mungu basi pia amekufuru na hakuna kufananisha katika sifa alizojisifia mwenyewe Mwenyezi Mungu au alizomsifia Mtume wake. Hivyo basi, yeyote anayemthibitishia Mwenyezi Mungu majina na sifa zilizokuja katika aya za wazi [za Qurani] na Hadithi sahihi [za Mtume] katika njia inayowiana na utukufu wa Mwenyezi Mungu na akazikanusha kasoro, basi huyo amefuata njia ya uongofu".<sup>xxix</sup>*

## **2. KUAMINI MALAIKA**

Kuamini Malaika kunajumuisha kuwaamini Malaika kwa ujumla na kwa ufanuzi. Hivyo, Muislamu anaamini kuwa Mwenyezi Mungu ana Malaika aliowaumba ili wamtii, na amewasifu kuwa wao ni: "Waja watukufu. Hawamtangulii kwa kauli na wanazitekeleza amri zake. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao na wala hawamuombei ila tu yule ambaye Mwenyezi Mungu amemridhia na wao (Malaika) kutokana na kumuogopa yeye (Mwenyezi Mungu) ni wanyenyekemu".<sup>xxx</sup>

Malaika wako aina nyingi. Miongoni mwao kuna waliopewa jukumu la kuibeba Arshi. Kuna watumishi wa سبحة الارواح - قسم الكتب

peponi na motoni na kuna waliopewa jukumu la kuyahifadhi matendo ya waja.

Tunawaamini kwa ufanuzi malaika ambao Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamewataja kwa majina, kama Jibrili, Mikail, Malik mtumishi wa motoni na Israafil aliyepewa jukumu la kupuliza parapanda na ambaye ametajwa katika Hadithi sahihi [za Mtume].

Imethibiti katika Hadithi sahihi iliyo nukuliwa kutoka kwa Aisha [Mke wa Mtume], Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Malaika wameumbwa kutokana na nuru na majini wameumbwa kutokana na wako la moto na ameumbwa Adamu kutokana na kile mllichotajiwa<sup>xxxii</sup>*".<sup>xxxii</sup>

### 3. KUAMINI VITABU

Ni wajibu kuamini kwa ujumla kwamba Mwenyezi Mungu aliyetakasika ameteremsha vitabu kwa Mitume wake ili kuiweka wazi haki na kuihubiri, kama Mwenyezi Mungu alivyosema kuwa: "*Hakika, tumewatuma Mitume wetu kwa hoja zilizo wazi na tumeteremsha pamoja nao vitabu na mizani ili watu wasimamie uadilifu*".<sup>xxxiii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka kuwa: "*Watu (wote) walikuwa ni umma mmoja (ulio katika dini moja ya haki aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu lakini halafu wakatafautiana), hivyo Mwenyezi Mungu akatuma Mitume wake wakitoa habari njema na wakitoa habari za maonyo, na akateremsha pamoja nao vitabu kwa haki ili (vitabu hivyo)*



*vihukumu baina ya watu katika yale waliyotafautiana".*<sup>xxxiv</sup>

شدة



Pia tunaviamini kwa ufanuzi vile vitabu alivyovitaja Mwenyezi Mungu. Miogoni mwa vitabu hivyo ni kama Torati, Injili, Zaburi na Qur'ani.

Qur'ani Tukufu ndio kitabu bora zaidi, cha mwisho, kinachovitawala vitabu vyote na ndicho kinachovisadikisha. Qur'ani, pamoja na Sunna sahihi zilizonukuliwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ndio mambo yanayoupasa umma wote kuyafuata na kutekeleza sheria zake. Hizo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu aliyetukuka amemleta Mtume wake Muhammad ili awe Mtume kwa watu na majini. Pia ameteremsha kitabu pamoja naye ili kitabu hicho kiwe hakimu kati ya watu na kukifanya kuwa ni dawa kwa magonjwa yaliyomo katika nyoyo. Pia Qur'an ni ufanuzi wa kila jambo, ni mwongozo na ni rehema kwa waumini, kama Mwenezyi Mungu alivyosema kuwa: "*Na hiki ni kitabu tulichokiteremsha, chenye baraka, hivyo kifuateni na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate rehema*".<sup>xxxv</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka kuwa: "*Na tumeteremsha kwako kitabu kikiwa ni ufanuzi wa kila jambo na ni mwongozo na ni rehema na ni habari njema kwa Waislamu (wanaomtii Mwenyezi Mungu)*".<sup>xxxvi</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Sema: Enyi watu, hakika mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (niliyetumwa) kwenu nyote, (Mwenyezi Mungu) ambaye ni wake yeye tu ufalme wa mbinguni na ardhini, hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila yeye tu, anayeleta uhai na mauti, hivyo muaminini*

شبكة الألوكة - قسم الكتب



*Mwenyezi Mungu na Mtume wake; Nabii asiyejua kusoma kilichoandikwa na asiyejua kuandika, Mtume ambaye anamuamini Mwenyezi Mungu na maneno yake, na mfuateni ili mpate kuongoka".<sup>xxxvii</sup>*

Aya za Qurani katika kuelezea maana hii ni nyingi sana.

#### 4. KUAMINI MITUME

Inapasa kuwaamini Mitume kwa ujumla na kwa ufafanuzi. Tunaamini kuwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka na kutakasika ametuma kwa waja wake Mitume wanaotokana na wao; Mitume wanaotoa habari njema na wanaotoa habari za maonyo na wanaohubiri haki. Yeyote anayewaitika Mitume atapata wema na yejote anayewapinga atapata hasara na majuto. Mtume wa mwisho na bora zaidi ni Mtume wetu Muhammad bin Abdallah. Amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka kuwa: "*Na hakika, tumepeleka katika kila umma Mtume (akiwa na ujumbe) kwamba muabuduni Mwenyezi Mungu na muepukeni Taaghruut*".<sup>xxxviii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka kuwa: "*(Tumewaleta) Mitume wanaotoa habari njema, wanaotoa habari za maonyo ili watu wasiwe na hoja kwa Mwenyezi Mungu baada ya (kuletewa) Mitume (hao)*".<sup>xxxix</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu alietyukuka kuwa: "*Muhammad sio baba wa yejote katika wanaume wenu, bali (yeye) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni Mtume wa mwisho*".<sup>xl</sup>

Mtume yejote ambaye Mwenyezi Mungu amemtaja katika Mitume hao au kutajwa kwake kumethibiti



kunukuliwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi tunamwamini kwa njia ya ufafanuzi na kuainisha; kama Mtume Nuhu, Huud, Saleh, Ibrahim na wengineo Mwenyezi Mungu awafikishie, pia amfikishie Mtume wetu, rehema na amani bora na tukufu.

## 5. KUAMINI SIKU YA MWISHO

Ama kuamini Siku ya Mwisho, huingia humo kuyaamini mambo yote yatakayotokea baada ya kufa; mambo ambayo Mwenyezi Mungu na Mtume wake wameyaeleza, kama mtihani wa kaburini (fit-natul-qabri); mateso na neema zake. Pia huingia humo kuamini yatakayotokea Siku ya Kiyama ikiwa ni pamoja na shida na mateso, siraat<sup>xli</sup>, mizani, kuhisabiwa, malipo, kutolewa vitabu kwa watu ambapo kuna atakayechukua kitabu chake kwa mkono wa kulia na kuna atakayechukua kitabu chake kwa mkono wa kushoto au nyuma ya mgongo wake. Pia huingia katika kuiamini Siku ya Mwisho kuamini Birika ya Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuamini pepo, moto, waumini kumuona Mola wao na kuzungumza naye na mambo mengine yasiyokuwa hayo na ambayo yametajwa katika Qurani Tukufu na Sunna sahihi za Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Ni wajibu kuyaamini yote hayo na kuyasadiki katika njia ambayo Mwenyezi Mungu na Mtume wake wameifafanua.



## 6. KUAMINI QADAR

Ama kuamini Qadar kunajumuisha kuamini mambo  
manne:

- 1) Mwenyezi Mungu ameyajua yaliyotokea na yatakayotokea. Anazijua hali za waja wake, riziki zao, muda wao wa kuishi, matendo yao na mambo yao mengine yasiyokuwa hayo. Hakuna chochote katika hayo kinachofichikana kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka, kama alivyosema kuwa: "*Hakika, Mwenyezi Mungu kwa kila kitu ni mjuzi*".<sup>xlii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "...ili mjue kuwa *Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kila kitu na kwamba Mwenyezi Mungu anakijua vyema kila kitu*".<sup>xliii</sup>
- 2) Jambo la pili ni kwamba, Mwenyezi Mungu amekiandika kila alichokikadiria na kukihukumu, kama alivyosema kuwa: "*Hakika, tunakijua kila kinachopunguzwa na ardhi kwao (katika miili yao wakati wanapooza makaburini) na kwetu kipo kitabu chenye kuhifadhi (kila kitu)*".<sup>xliv</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Na kila kitu tumekihifadhi katika kitabu chenye kubainisha (kila kitu)*".<sup>xlv</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Hivi hujui kwamba, Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo katika mbingu na ardhi? Hakika, hilo lipo katika kitabu. Hakika, hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jepesi*".<sup>xlvii</sup>
- 3) Jambo la tatu ni kuamini utashi wa Mwenyezi Mungu unaoendelea. Anayoyataka Mwenyezi huwa na



asiyoyataka hayawi, kama alivyosema kuwa: "*Hakika, Mwenyezi Mungu hufanya anayoyataka*".<sup>xlvii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kwamba: "*Hakika, hapana vingine isipokuwa kwamba amri yake (Mwenyezi Mungu) akitaka jambo ni kuliambia 'kuwa' na (hapo hapo) huwa*".<sup>xlviii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Na (wala nyinyi) hamtaki ila tu atake Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu*".<sup>xlix</sup>

- 4) Jambo la nne ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa vyote vilivyopo. Hakuna Muumba wala Mola isipokuwa yeze tu, kama alivyosema kuwa: "*Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu na yeze ndiye Mlinzi wa kila kitu*".<sup>l</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "*Enyi watu, zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu kwenu. Hivi kuna Muumba yeyote (mwengine) asiyekuwa Mwenyezi Mungu anayewaruzuku nyinyi kutoka mbinguni na ardhini? Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa yeze (Mwenyezi Mungu) tu. Vipi basi mapotoshwa?*"<sup>li</sup>

Kwa watu wa Sunna na Jamaa, kuamini Qadar kunajumuisha kuamini mambo yote haya manne, kinyume cha baadhi ya watu wa Bid'a wanaokanusha baadhi ya mambo hayo.

Inaingia katika kumuamini Mwenyezi Mungu kuitakidi kuwa imani ni maneno na vitendo. Imani inaongezeka kwa utiifu na inapungua kwa kufanya maasi. Pia haifai kumfanya Muislamu yeyote kuwa ni kafiri kwa sababu

ya kutenda jambo lolote katika maasi ambayo sio Shirk na sio Ukarifi, kama: [www.alukah.net](http://www.alukah.net) zinaa, wizi, kula riba, kunywa ulevi, kuwadharau wazazi na madhambi mengine makubwa yasiyokuwa hayo, madamu Muislamu huyo hajakuwa na itikadi kwamba madhambi hayo ni halali. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika isemayo kwamba: "*Hakika, Mwenyezi Mungu hana msamaha katika kushirikishwa (naye kitu chochote) na anasamehe dhambi isiyokuwa hiyo (ya shirki) kwa anayemtaka*".<sup>lii</sup> Hii pia ni kwa mujibu wa vile ilivyothibiti katika Hadithi zilizonukuliwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba, Mwenyezi Mungu atamtoa katika moto kila ambaye katika moyo wake mna chembe ndogo ya imani.

Ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kufanya urafiki kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kufanya uadui kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Muumini anatakiwa awapende Waumini na kuwafanya marafiki, awachukie makafiri na kuwafanya maadui.<sup>liii</sup>

Waumini wakubwa wa Umma huu ni Swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Watu wa Sunna na Jamaa wanawapenda Swahaba, wanawafanya marafiki na wana itikadi kwamba wao ni watu bora zaidi baada ya Mtume, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: "*Karne bora zaidi ni karne yangu, halafu ni wale ambao wanawafuatia hao, halafu ni wale ambao wanawafuatia hao*".<sup>liv</sup>

Watu wa Sunna na Jamaa wana itikadi pia kwamba, Swahaba bora zaidi ni Abubakar As-siddiq, halafu Omar Al-



faaruuq, halafu Othmaan Dhun-nuurain, halafu Aliy Al-murtadhaa, Mwenyezi Mungu awawiye radhi wote. Baada ya hao ni Swahaba waliosalia kati ya Sahaba kumi waliokwishapewa habari njema ya kupata pepo, halafu ni Swahaba waliosalia. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awawiye radhi wote.

Watu wa Sunna na Jamaa wanazinyamazia tafuati zilizojitokeza kati ya Swahaba na kuitakidi kuwa Swahaba katika kutafautiana huko walikuwa wakijitahidi. Mwenye kupatia ana malipo mara mbili na mwenye kukosea ana malipo mara moja.

Watu wa Sunna na Jamaa wanawapenda watu wa familia ya Mtume (Ahlul-bait) wanaomwamini Mtume; wanawapenda wao na pia wanawapenda na kuwaenzi wake wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaa ni mama wa Waumini, na wanawaombea radhi wote.

Watu wa Sunna na Jamaa wanajiepusha na mwenendo wa Raafidhah<sup>lv</sup> ambaa wanawachukia Swahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuwatukana. Pia wanachupa mipaka kwa watu wa familia ya Mtume na kuwatukuza zaidi ya daraja aliywapa Mwenyezi Mungu. Aidha watu wa Sunna na Jamaa wanajitenga na mwenendo wa Nawaasib wanaowaudhi watu wa familia ya Mtume kwa kauli au vitendo.

Maneno yote haya mafupi tuliyoyataja kuhusu itikadi sahihi ambayo kwayo Mwenyezi Mungu amemtuma Mjumbi wake Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ndio itikadi ya kikundi kilicho okoka; Watu wa Sunna na Jamaa, kikundi ambacho Mtume amekielezea kwa kusema kuwa: "*Halitaacha kundi katika umma wangu kuwa juu ya haki ni lenye kunusuriwa. Hatowadhuru mwenye kuwafedhehesha mpaka*

*ije amri ya Mwenyezi Mungu (Kiyama)". Pia amesema Mtume kuwa: "Wamegawanyika Wayahudi katika vikundi sabini na moja na wamegawanyika Wakristo katika vikundi sabini na mbili na utagawanyika umma huu (wa Kiislamu) katika vikundi sabini na tatu. Vikundi vyote vitaingia motoni isipokuwa kimoja. Swahaba wakauliza: Ni kipi kikundi hicho ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Akajibu Mtume kuwa: Ni wale watakaokuwa katika mfano wa yale mambo niliyonayo mimi na Swahaba wangu".*

Hiyo ndiyo itikadi sahihi ambayo inapasa kushikamana nayo, kuidumisha na kujihadhari na kila jambo lililo dhidi yake.

Ama waliojitenga na Itikadi hii na kwenda kinyume nayo wako aina nyingi. Kuna wanaoabudu masanamu, Malaika, mawalii, majini, miti, mawe n.k. Hawa hawakuuitika wito wa Mitume bali wamewapinga na kuwafanya inda, kama walivyofanya Waquraish na Waarabu wengine kwa Mtume wetu Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Vitu walivyokuwa wakiviabudu Waquraish na Waarabu walikuwa wakiviomba kuwatatalilia shida, kuponya wagonjwa na kupata ushindi kwa maadui. Pia walikuwa wakichinja na kuvivekea nadhiri hivyo walivyokuwa wakiviabudu. Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alipowakataza kufanya hivyo na kuwaamuru waitakase ibada kwa Mwenyezi Mungu pekee walilishangaa hilo, walilikataa na kusema kwamba: "*Hivi (huyu Muhammad) amewafanya Miungu (wote) kuwa*



*Mungu mmoja? Hakika, hili ni jambo la ajabu sana!*<sup>lvii</sup>

Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, hakuacha kuhuwahubiria watu waelekee kwa Mwenyezi Mungu, kuwatahadharisha na Shirki na kuwafafanulia uhakika wa mahubiri (daawah) aliyokuwa akiwahubiria mpaka Mwenyezi Mungu akawaongoza aliowaongoza mionganoni mwao. Halafu watu waliingia katika dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi. Dini ya Mwenyezi Mungu ikazishinda dini nyingine baada ya mahubiri ya mfululizo na juhud (Jihad) ndefu kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Swahaba wake na waliowafuatia hao kwa wema.

Hali baadae ilibadilika na watu wengi wakakumbwa na ujinga mpaka wengi wao wakarudi kwenye dini ya ujinga (Jaahiliyyah) kwa kuchupa mipaka katika kuwaadhimisha Mitume na mawalii kwa kuwaomba, kuwataka msaada na aina nyingine za ushirikina zisizokuwa hizo. Watu hawakujua maana ya 'Laa ilaaha Illa-Laah' kama makafiri wa Kiarabu walivyojua maana yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu msaada!

Shirki hii bado ingali ikienea kati ya watu hadi wakati wetu huu, kwa sababu ya kuzidiwa na ujinga na kuwa mbali na kipindi cha utume. Dhana ya hawa waliokuja nyuma ni dhana ile ile ya watu wa mwanzo. Dhana hiyo ni kule kusema kwao kuwa: "*Hawa (tunao waomba) ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu*".<sup>lviii</sup> "*Hatuwaabudu isipokuwa tu kwa kutaka watufanye tuwe karibu na Mwenyezi Mungu*".<sup>lviii</sup> Mwenyezi Mungu ameibatilisha dhana hii na kufafanua kuwa, mtu yejote anayemuabudu asiyekuwa Mwenyezi



Mungu vyovyote awavyo, basi mtu huyo amemfanyia Mwenyezi Mungu shirki (ushirika) na amekuwa kafiri, kama Mwenyezi Mungu alivyosema kuwa: "*Na wanaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu, (vitu) visivyowadhuru (endapo hawatoviabudu) na visivyowanufaisha (endapo wataviabudu) na wanasema: Hawa ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu*".<sup>lx</sup> Mwenyezi Mungu amewajibu kwa kusema kuwa: "Sema: *Hivi mnamuambia Mwenyezi Mungu mambo asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi? Mwenyezi Mungu ametukuka na ametakasika na (hayo) wanayoshirikisha*".<sup>lx</sup>

Katika aya hizi Mwenyezi Mungu amebainisha kuwa, kumuabudu asiyekuwa yeye ikiwa ni Mitume au mawalii au wengine ni Shirki kubwa sana, japo wanaoifanya wataiita kwa jina jingine. Pia Mwenyezi Mungu amesema kuwa: "*Na wale amba o huwafanya wasiokuwa yeye (Mwenyezi Mungu) kuwa ni wapenzi (husema): Hatuwaabudu isipokuwa tu kwa kutaka watufanye tuwe karibu na Mwenyezi Mungu*".<sup>lxii</sup> Mwenyezi Mungu amewajibu kwa kusema kuwa: "*Hakika, Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao katika yale ambayo wao wanahitalifiana. Hakika, Mwenyezi Mungu hamuongozi mtu ambaye yeye ni muongo, kafiri*".<sup>lxiii</sup> Kwa kauli hiyo, Mwenyezi Mungu ameweza wazi kuwa ibada yao ya kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu kwa kuomba, kuogopa, kutaraji na ibada nyingine kama hizo ni kumkufuru Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu amebainisha



kuwa ni waongo katika kusema kwao kuwa Miungu yao inawaweka karibu na yeye.

Miongoni mwa itikadi za kikafiri zinazopingana na itikadi sahihi na kutafautiana na yale waliyokuja nayo Mitume ni itikadi wanazoitakidi makafiri katika wakati wetu wa sasa, makafiri ambao ni wafuasi wa Marks na Lenin na wahubiri wengine wa ukafiri wasiokuwa hao. Ni sawa waziite itikadi hizo Ujamaa au Ukomunisti au Baath<sup>lxiii</sup> au majina mengine. Miongoni mwa misingi ya makafiri hawa ni kuwa hakuna Mungu na maisha ni uyakinifu (material). Miongoni mwa misingi yao pia ni kukanusha kuwepo kwa Akhera, pepo, moto na kuzikanusha dini zote. Yeyote atakayevitupia macho vitabu vyao na kuyapitia mambo yao atalijua hilo kwa yakini. Ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba, itikadi hii inapingana na dini zote na inawapeleka wafuasi wake kwenye mwisho mbaya duniani na Akhera.

Miongoni mwa itikadi zinazopingana na itikadi sahihi ni itikadi wanayoitakidi baadhi ya Al-Baatiniyyah<sup>lxiv</sup> na baadhi ya watu wa Tasawwuf<sup>lxv</sup> kwamba, baadhi ya watu wanaowaita mawalii (wapenzi wa Mungu) wanashirikiana na Mwenyezi Mungu katika matendo na kuwa na taathira katika mambo ya ulimwengu. Wanawaita mawalii hao Aqtaab, Autaad (nguzo/vizingi), Agh-waath (waokozi) na majina mengine waliyowaundia miungu yao hiyo. Hii ni shirki mbaya sana katika Rububiyya (matendo ya Mungu). Shirki hiyo ni mbaya zaidi kuliko shirki ya Waarabu wa wakati wa Ujaahiliyyah (ujinga wa dini). Makafiri wa Kiarabu hawakufanya shirki katika matendo ya Mwenyezi Mungu (Rububiyyah) bali walifanya shirki katika kuabudu (Uluhiyyah). Shirki yao pia ilikuwa katika wakati wa raha tu, ama katika wakati wa shida walikuwa wakimtakasia Mwenyezi Mungu ibada, kama alivyosema Mwenyezi

Mungu aliyetakasika kwamba: "Na pindi wakipanda katika majahazi (na kukumbwa na misukosuko) humuomba Mwenyezi Mungu huku wakimtakasia yeye dini, na pindi akiwaokoa na kuwafikisha nchi kavu basi wao hushirikisha".<sup>lxvi</sup>

Ama matendo ya Mwenyezi Mungu (Rubuubiyya) makafiri wa Kiarabu walikuwa wakikiri kwamba ni ya Mwenyezi Mungu pekee, kama Mwenyezi Mungu alivyosema kuwa: "Na kwa yakini, ukiwaauliza kwamba: Ni nani aliyewaumba? Kwa yakini, watasema kwamba: Ni Mwenyezi Mungu".<sup>lxvii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "Sema (uwaulize kwamba): Ni nani anayewaruzuku kutoka mawinguni na ardhini au ni nani anayemiliki usikivu (masikio) na uoni (macho) na ni nani anyetoa kilicho hai kutokana na kilichokufa na kutoa kilicho kufa kutokana na kilicho hai na ni nani anaye endesha mambo (ya ulimwengu)? Watasema kwamba: Ni Mwenyezi Mungu. Sema (uwaambie): Hivi hamumchi Mungu?".<sup>lxviii</sup> Aya nyingine katika kuelezea maana hii ni nyingi.

Ama washirikina wa baadaye wamewazidi washirikina wa mwanzo katika sehemu mbili:-

- 1) Baadhi yao wamefanya shirki katika matendo ya Allah (Rubuubiyyah).
- 2) Shirki yao inafanyika katika wakati wa raha na wakati wa shida, kama ambavyo anaweza akayajua hayo mtu

atakayejumuika nao, akachunguza hali zao na kuona wanayoyafanya katika kaburi la Hussein, Badawiy na makaburi mengine huko Misri, kaburi la Aidaruus huko Aden (Yemen), kaburi la Al-Haadiy huko Yemen, kaburi la Ibn-Arabiyy huko Shaam (Syria), kaburi la Sheikh Abdulqadir Al-Jeylaniy huko Iraq na makaburi mengine mashuhuri ambayo watu wengi wamechupa mipaka katika kuyaadhimisha na kuyapa haki nyingi za Mwenyezi Mungu.

Ni wachache wanaoyakataza hayo na kuwabainishia watu hakika ya Tawhiid (kumpwekesha Mungu) ambayo kwa Tawhiid hiyo Mwenyezi Mungu amemtuma Mjumbe wake Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na Mitume wengine kabla yake, Mwenyezi Mungu awafikishie rehema na amani. Innaa lilleah Wain-naa ilaihi raajiuun. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awarudishe wanaofanya hayo kwenye uongofu, awapeleke kwa wingi kati yao wahubiri wa uongofu na awasadie viongozi wa Waislamu na Wanazuoni wao ili waipige vita shirki hii na kuiangamiza. Hakika, ye ye Mwenyezi Mungu ni msikivu, aliye karibu.

Miongoni mwa itikadi zinazopingana na itikadi sahihi katika mlango wa majina na sifa za Mwenyezi Mungu ni itikadi za watu wa Bid'a (uzushi) ikiwa ni pamoja na Jahmiyya<sup>lxix</sup>, Muutazila<sup>lxx</sup> na wanaowafuata hao katika kuzikana sifa za Mwenyezi Mungu, kumtenga Mwenyezi Mungu na sifa za ukamilifu na kumsifu kwa sifa za visivyokuwepo, visivyokuwa na uhai na vilivyo muhalii. Ametakasika Mwenyezi Mungu na maneno yao kutakasika kukubwa.



Pia huingia katika mkumbo huo wale wanaokana baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu na kuthibitisha baadhi yake, kama Ashaairah<sup>lxxi</sup>. Inawalazimu katika sifa walizozithibitisha mfano wa hoja walizozikimbia katika sifa walizozikana na kuzipotosha ushahidi wake. Kwa kufanya hivyo, wamezipinga hoja za kunukuliwa (Qur'an na Hadithi za Mtume) na za kiakili, na wamejikanganya kujikanganya kuliko wazi.

Ama Watu wa Sunna na Jamaa wao wamemthibitishia Mwenyezi Mungu sifa na majina aliyojithibitishia ye ye mwenyewe au kuthibitishiwa na Mtume wake Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwa njia ya ukamilifu. Pia wamemtakasa Mwenyezi Mungu na kufanana na viumbe vyake kutakasa kusikokuwa na kukana maana (Taatiil). Hivyo, wamezitumia hoja zote na hawakupotosha wala kukanusha maana. Wamesalimika na mkanganyo ambao wengine wametumbukia katika mkanganyo huo, kama uliyotangulia ufanuzi wa hayo. Hii ndiyo njia ya uokovu na wema katika dunia na akhera na ndiyo njia iliyonyooka na ambayo ilifuatwa na maimamu na Salaf (Wema Waliotangulia) wa umma huu. Hakuna kitakachowafanya wawe wema watu wa mwisho wa umma huu isipokuwa tu kwa kufuata kile kilichowafanya kuwa wema watu wa mwanzo wa umma huu na ambacho ni kufuata Qur'an na Sunna na kuacha yanayokwenda kinyume na viwili hivyo.



## MAMBO YANAYOTENGUA UISLAMU

Ndugu yangu Muislamu, jua kwamba Mwenyezi Mungu aliyetakasika amewajibisha kwa waja wote kuingia katika Uislamu, kushikamana nao na kujihadhari na kila linalokwenda kinyume na Uislamu. Mwenyezi Mungu pia amemtuma Mtume wake Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ili kulihubiri hilo. Aidha Mwenyezi Mungu amefahamisha kuwa yejote anayemtii yejye ameongoka na yejote anayempinga amepotea. Katika aya nyingi Mwenyezi Mungu amehadharisha sababu za kuritadi (kutoka katika Uislamu) na aina nyingine za shirki na ukafiri. Wanazuoni pia, Mwenyezi Mungu awarehemu, katika mlango wa hukumu ya Murtadd (mtu aliyotoka katika Uislamu) wametaja kwamba, Muislamu anaweza kutoka katika dini yake kwa kutenda aina nyingi ya mambo yanayo halalisha damu yake (kwa kuuawa) na mali yake (kwa kutaifishwa). Kwa kutenda mambo hayo, mtu anakuwa yuko nje ya Uislamu. Hatari zaidi katika mambo hayo na ambayo hutokea sana ni mambo kumi. Katika maelezo yafuatayo tutakutajia mambo hayo kwa ufupi ili ujihadhari nayo na pia umhadharishe mwenzako kwa kutaraji salama na uzima wa kuepukana nayo. Pamoja na hayo, utatajwa ufanuzi kidogo baada yake.

- 1) La kwanza katika mambo kumi yanayotengua Uislamu ni kufanya shirki (ushirika) katika kumuabudu Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka kwamba: "*Hakika, Mwenyezi Mungu hana msamaha katika kushirikishwa naye (kitu chochote) na*



*anasamehe dhambi isiyokuwa hiyo kwa anayemtaka*"<sup>lxxii</sup> Na amesema Mwenyezi Mungu kuwa: "Hakika, ilivyo ni kwamba, ye yote anayemshirikisha Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu ameharamisha juu yake pepo na makazi yake ni motoni na madhalimu hawana watetezi"<sup>lxxiii</sup> Ni mionganini mwa shirki kuwaomba watu waliokufa, kuwataka uokovu, kuweka nadhiri na kuchinja kwa ajili yao.

- 2) Jambo la pili ni kwamba, mtu ye yote anayeweka kati yake na kati ya Mwenyezi Mungu wakaakati (mediators) anaowaomba, kuwataka uombezi na kuwategemea basi mtu huyo amekufuru, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni wote.
- 3) Jambo la tatu ni kwamba, mtu ye yote asiyekubali itikadi kwamba makafiri ni makafiri au akiutilia shaka ukafiri wao au akiwa na itakadi kwamba madhehebu yao ni sahihi, basi mtu huyo amekufuru.
- 4) Jambo la nne ni kwamba, mtu ye yote anayekuwa na itikadi kwamba muongozo usiokuwa wa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni mkamilifu zaidi kuliko wa Mtume au kwamba sheria zisizokuwa za Mtume ni nzuri zaidi kuliko sheria zeke, kama wale wanaoona kuwa sheria za Taghuti ni bora kuliko sheria zake, basi mtu huyo ni kafiri.
- 5) Jambo la tano ni kwamba, mtu ye yote anayechukia jambo katika mambo aliyokuja nayo Mtume japokuwa analitekeleza, basi mtu huyo amekufuru kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka isemayo kuwa: "*Hiyo ni kwa sababu*



*wao (makafiri) wameyachukia yale  
aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, hivyo  
akaziporomosha amali zao".*

الله  
الله

- 6) Jambo la sita ni kwamba, mtu yejote anayelifanya istihzai (dharau) jambo lolote katika dini ya Mtume au thawabu zake au mateso yake, basi mtu huyo amekufuru. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka isemayo kuwa: "*Sema (uiwaambie kwamba): Hivi Mwenyezi Mungu na aya zake na Mtume wake mlikuwa mnafanyia istihzai? Msiombe radhi, kwani hakika mmekufuru baada ya imani yenu*".<sup>lxxv</sup>
- 7) Jambo la saba ni uchawi. Miongoni mwa uchawi ni As-Sarf<sup>lxxvi</sup> na Al-Atf<sup>lxxvii</sup>. Mtu yejote mwenye kufanya hayo au akayaridhia basi amekufuru. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu alietyukuka isemayo kwamba: "*Na hawamfundishi yejote (uchawi) mpaka waseme: Hapana vingine isipokuwa kwamba sisi ni fitina (mtihani) hivyo, usikufuru*".<sup>lxxviii</sup>
- 8) Jambo la nane ni mtu kusaidiana na kushirikiana na makafiri dhidi ya Waislamu. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu alietyukuka isemayo kuwa: "*Na yejote anayewafanya wao urafiki (wa ndani) katika nyinyi basi yeye ni katika wao. Hakika, Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu*".<sup>lxxix</sup>
- 9) Jambo la tisa ni kwamba, mtu yejote ambaye ana itikadi kwamba baadhi ya watu wana hiyari ya kutoka katika sheria ya Mtume Muhammad, basi mtu huyo ni kafiri, kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu



Mtukufu isemayo kwamba: "*Na ye yeyote anayetaka usiokuwa Uislamu kuwa ndiyo dini, basi hataku baliwa na yeye akhera atakuwa mionganini mwa wenye hasara*".<sup>lxxx</sup>

- 10) Jambo la kumi ni kuipuuza dini ya Mwenyezi Mungu; kwa maana kwamba mtu hajifunzi dini wala haitekelezi. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "*Na ni nani dhalimu zaidi kuliko ambaye amekumbushwa kwa aya za Mola wake halafu akazipuuza? Hakika, sisi tutawaadhibu madhalimu*".<sup>lxxxi</sup>

Hakuna tafauti katika mambo yote hayo yanayotengua Uislamu kati ya mtu anayefanya mzaha, anayefanya kweli na anayefanya kwa woga, isipokuwa tu mtu aliyetenzwa nguvu. Mambo yote haya ni mionganini mwa mambo hatari sana na yanayotokea sana. Inatakikana kwa Muislamu ajihadhari nayo na kuyaogopa, kwa usalama wake.

Na anaingia katika lile jambo la nne mtu anayekuwa na itikadi kwamba:

- Mifumo na sheria wanazoziweka watu ni bora zaidi kuliko sheria za Kiislamu, au kwamba:
- Mfumo wa Kiislamu haufai kutekelezwa katika karne ya ishirini, au kwamba:
- Mfumo wa Kiislamu ndio uliosababisha Waislamu kuwa nyuma, au kwamba:
- Uislamu uhusishwe tu na uhusiano kati ya mtu na Mola wake bila ya kuingilia mambo mengine ya maisha.



Aidha anaingia katika lile jambo la nne mtu anayeona kuwa, kutekeleza sheria ya Mwenyezi Mungu katika kukata-mkono wa mwizi au kumpiga mawe mzinifu aliyehifadhika ni jambo lisilowiana na wakati wa sasa.

Pia anaingia katika fungu hilo kila mtu mwenye itikadi kwamba, inafaa kutumia sheria zisizokuwa za Mwenyezi Mungu katika Muaamalaat (mambo yasiyo ya kiibada) na adhabu (huduud) au mengineyo, hata kama hakuitakidi kuwa sheria hizo ni bora zaidi kuliko sheria za Mwenyezi Mungu. Hii ni kwa sababu, kwa itikadi yake hiyo, atakuwa amehalalisha mambo aliyyaharamisha Mwenyezi Mungu. Kila anayehalalisha aliyyaharamisha Mwenyezi Mungu katika mambo yanayojudikana katika dini kwa lazima kama zinaa, pombe, riba na kuhukumu kwa kutumia sheria zisizokuwa za Mwenyezi Mungu, basi mtu huyo ni kafiri kwa makubaliano ya wanazuoni wote.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde na mambo yanayosababisha hasira zake na adhabu yake chungu. Pia tunamuomba Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani kiumbe wake bora zaidi Muhammad, Jamaa na Swahaba wake.



<sup>i</sup> Sunna ni kila jambo sahihi linalo husishwa na Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, iwe ni kauli au vitendo au nyamazio (Mtume kupata habari kuwa jambo fulani limefanywa naye asiseme lolote akanyamaza).

<sup>ii</sup> Sura Al-Maaida(5), aya 5.

<sup>iii</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 65.

<sup>iv</sup> Mambo ya kitiikadi yasiyo onekana.

<sup>v</sup> Sura Al-Baqara(2), aya 177.

<sup>vi</sup> Sura Al-Baqara(2), aya 285.

<sup>vii</sup> Sura An-Nisaa(4), aya 136.

<sup>viii</sup> Sura Al-Hajj(22), aya 70.

<sup>ix</sup> Ameipokea Hadithi hii Imam Muslim

<sup>x</sup> Sura Adh-Dhaariyaat(51), aya 56-58.

<sup>xi</sup> Sura Al-Baqara(2), aya 21-22.

<sup>xii</sup> Taghuti ni kila kitu kinacho abudiwa na kikawa radhi juu ya kuabudiwa huko.

<sup>xiii</sup> Sura An-Nahli(16), aya 36.

<sup>xiv</sup> Sura Al-An'biyaa(21), aya 25.

<sup>xv</sup> Sura Huud(11), aya 1-2.

<sup>xvi</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 2-3.

<sup>xvii</sup> Sura Al-Israa/Banii-Israa'il(17), aya 23.

<sup>xviii</sup> Sura Ghaafir/Al-Muumin(40), aya 14.

<sup>xix</sup> Ameipokea Hadithi hii Imam Bukhari na Imam Muslim.

<sup>xx</sup> Sura Luqmaan(31), aya 30.

<sup>xxi</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 62.

<sup>xxii</sup> Sura Al-Aaraaf(7), aya 54.

<sup>xxiii</sup> Sura Ash-Shuuraa(42), aya 11.

<sup>xxiv</sup> Sura An-Nahli(16), aya 74.

<sup>xxv</sup> Jawabu hilo lipo kwenye kijitabu na kina itwa 'Ar-Risaalah Al-Hamawiyah'.

<sup>xxvi</sup> Sura Al-An'biyaa(21), aya 18.

<sup>xxvii</sup> Sura Al-Furqaan(25), aya 33.

<sup>xxviii</sup> Sura Al-Aaraaf(7), aya 54.

<sup>xxix</sup> Ibn-Kathiir,Tafsir, Sura Al-Aaraaf(7), aya 54.  
سبحة الارواح - قسم الكتب

<sup>xxx</sup> Sura Al-An'biyaa(21), aya 26-28.

<sup>xxxi</sup> Tulichotajiwa ni kwamba Mtume Adamu ameumbwa kutokana na udongo.Tazama Qur'an,kwa mfano,sura As-Sajda(32), aya 7 au sura Saad(38), aya 71.

<sup>xxxii</sup> Ameipokea Hadithi hii Imam Muslim.

<sup>xxxiii</sup> Sura Al-Hadiid(57), aya 25.

<sup>xxxiv</sup> Sura Al-Baqara(2), aya 213.

<sup>xxxv</sup> Sura Al-An'aam(6), aya 155.

<sup>xxxvi</sup> Sura An-Nahl(16), aya 89.

<sup>xxxvii</sup> Sura Al-Aaraaf(7), aya 158.

<sup>xxxviii</sup> Sura An-Nahl(16), aya 36.

<sup>xxxix</sup> Sura An-Nisaa(4), aya 165.

<sup>xl</sup> Sura Al-Ahzaab(33), aya 40.

<sup>xli</sup> Siraat ni njia nyembamba watakayo tahiniwa watu kwa kupita kwenda peponi.

<sup>xlii</sup> Sura Al-Mujaadila(58), aya 7.

<sup>xliii</sup> Sura At-Talaaq(65), aya 12.

<sup>xliv</sup> Sura Qaaf(50), aya 4.

<sup>xlv</sup> Sura Yaasiin(36), aya 12.

<sup>xlivi</sup> Sura Al-Hajj(22), aya 70.

<sup>xlvii</sup> Sura Al-Hajj(22), aya 18.

<sup>xlviii</sup> Sura Yaasiin(36), aya 82.

<sup>xlix</sup> Sura At-Takwiir(81), aya 29.

<sup>1</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 62.

<sup>li</sup> Sura Faatir(35), aya 3.

<sup>lii</sup> Sura An-Nisaa(4), aya 116.

<sup>liii</sup> Tazama kwa mfano Sura Al-Mujaadila(58), aya 22 au Sura Al-Mumtahina(60), aya 1-6.

<sup>liv</sup> Ameipokea Hadithi hii Imam Muslim.

<sup>lv</sup> Raafidha ni mionganini mwa vikundi nya Shia. Mionganini mwa itikadi za kikundi hiki ni kuamini kuwa Swahaba Alliy bin Abi-Talib alipewa usia na Mtume kwamba awe kiongozi wa Waislamu baada ya kufa kwa Mtume. Kwa msingi huo, kikundi hiki kina itikadi kwamba Swahaba wengi, akiwemo Abubakar, Omar na Othman watu ambao hawakumpa Alliy uongozi baada ya kufa Mtume ni madhalimu.

<sup>lvi</sup> Sura Saad(38), aya 5.



<sup>lvii</sup> Sura Yunus(10), aya 18.

<sup>lviii</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 3.

<sup>lix</sup> Sura Yunus(10), aya 18.

<sup>lx</sup> Sura Yunus(10), aya 18.

<sup>lxi</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 3.

<sup>lxii</sup> Sura Az-Zumar(39), aya 3.

<sup>lxiii</sup> Baath ni nadharia ya kisiasa iliyoanzishwa katika nchi za Kiarabu. Pamoja na malengo mengine, nadharia hii ina madhumuni ya kuleta umoja wa Kiarabu, uhuru na ujamaa.

<sup>lxiv</sup> Baatiniyya ni mojawapo ya madhehebu ya Shia. Wafuasi wa madhehebu haya huamini kuwa, sheria za Qur'an Tukufu zina nje (dhaahir) na ndani (baatin). Nje ya sheria hizo sio makusudio bali makusudio ni ndani ambayo haifahamiki isipokuwa tu kuititia kwa kiongozi aliyekingwa asitende dhambi (Imam maasoum).

<sup>lxv</sup> Tasawwuf, wafuasi wake wakijulikana kama Suufiy, ni nadharia ya kiitikadi ambayo mionganoni mwa malengo yake ni kumtaka muumini aelekee kwa Mungu tu na kujiepusha na mambo ya kilimwengu. Pia wafuasi wa nadharia hii wanaamini kwamba dini ni nje na ndani. Nje ni matendo ambayo hutendwa na kila mtu na ndani ni daraja ya juu ambayo hawaifiki daraja hiyo isipokuwa tu wateule (mawalii) maalumu.

<sup>lxvi</sup> Sura Al-Ankabuut(29), aya 65.

<sup>lxvii</sup> Sura Az-Zukhruf(43), aya 87.

<sup>lxviii</sup> Sura Yunus(10), aya 31.

<sup>lxix</sup> Jahmiyya ni nadharia ya kiitikadi ambayo pamoja na mambo mengine wafuasi wake wanaitakidi kwamba Imani ni itikadi ya moyoni tu ya kumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake hata kama mtu hakuithibitisha imani hiyo kwa kutamka na kutekeleza faradhi.

<sup>lxx</sup> Muutazila ni kikundi kimojawapo kilichojitenga na itikadi sahihi. Mionganoni mwa itikadi zao ni kwamba, matendo ya mwanadamu yanatokana na yeye mwanadamu mwenyewe na wala sio kwa Qadari, Utashi na Uwezo wa Mwenyezi Mungu. Pia wao huzikanusha baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu.

<sup>lxxi</sup> Ashaaira ni wafuasi wa Imam Abulhasan Al-Ash'ariy kabla ya kurudi kwake katika itikadi ya Watu wa Sunna na Jamaa. Awali, Imam Abulhasan Al-Ash'ariy alikuwa katika itikadi ya Muutazila, lakini baadae aliikana itikadi hiyo na kurudi katika itikadi sahihi ya watu wa Sunna na



Jamaa. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba wanaojinasibisha na imamu huyu wanamfuata katika nadharia za kiiikadi za awali ambazo yeye mwenyewe baadae amezikataa.

Ixxiii Sura An-Nisaa(4), aya 116.

Ixxiii Sura Al-Maida(5), aya 72.

Ixxiv Sura Muhammad(47), aya 9.

Ixxv Sura At-Tauba(9), aya 65-66.

Ixxvi As-Sarf ni vitendo vya kichawi ambavyo hukusudiwa kwavyo kumbadilisha mtu katika jambo analolipenda, kama vile kumfanya mtu asimpende mkewe.

Ixxvii Al-Atf ni vitendo vya kichawi ambavyo hukusudiwa kwavyo kumfanya mtu apende jambo asilolipenda kwa kutumia njia za kishetani.

Ixxviii Sura Al-Baqara(2), aya 102.

Ixxix Sura Al-Maida(5), aya 51.

Ixxx Sura Aal-Imran(3), aya 85.

Ixxx Sura As-Sajda(32), aya 22.



هذا الكتاب منشور في

